mbalimbali waliojitokeza katika Viwanja vya Uhuru Park mijini Moshi juzi, wakati wa Maonyesho ya Wiki ya Kilimo Kanda ya Kaskazini yanayoendelea mjini hapo kwa kuratibitiwa na kampuni hiyo. **PICHA: JAMES LANKA**

NIPASHE UK 9

# *Wafugaji waonyeshwa fursa ya mifugo*

**Na Mbaraka Kambona,**
RUFIJI

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amewataka wafugaji wa Mkoa wa Pwani kuanza kuvuna mifugo yao na kuiuza, kwani kwa kufanya hivyo kutawasaidia kuwaongezea kipato na kupunguza migogoro kati yao na watumiaji wengine wa ardhi.

Ulega aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza na wafugaji na wakulima wa Wilaya ya Rufiji alipofanya ziara ya kusikiliza kero zao na kuzitafutia ufumbuzi.

Alisema ni muhimu viongozi wa wilaya za Rufiji, Mkuranga na Kibiti kukaa na wadau wa mifugo kutengeneza mkakati wa kuhamasisha uvunaji wa mifugo yao kwa kuwa soko la kuuza lipo mkoani humo na bado hawajalitumia ipasavyo.

"Hapa Mkoa wa Pwani tuna Kiwanda cha Nyama cha Tan-Choice, lakini pamoja na kiwanda hicho kuwapo hakuna mifugo inayopelekwa pale kutoka ukanda wetu huu wa Pwani," alisema Ulega.

Aliongeza kuwa ili faida ya uwapo wa kiwanda hicho ionekane, hivyo ni vyema wadau wote wa mifugo mkoani humo waanze uvunaji mkubwa na kupeleka kuiuza kiwandani hapo.

"Tunatamani kuona mifugo inatoka katika ukanda huu wa Pwani na kwenda kuuzwa jijini Dar es Salaam ambapo ndipo kwenye biashara kubwa ya nyama, msione fahari kukaa na makundi makubwa ya mifugo ambayo mwisho wa siku yakaonekana kuwa ni kero na hayana faida," aliongeza Ulega.

Kuhusu kuboresha huduma za mifugo, Waziri Ulega alisema kuwa katika Bajeti ya Mwaka huu 2021/ 2022 serikali imepanga kununua pikipiki 300 na itazigawa kwa maofisa ugani nchi nzima, ili waweze kutoa huduma ya mifugo kwa ufanisi.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Meja Edward Gowelle, alisema kufuatia migogoro mingi iliyoibuka, ameanzisha sensa ya mifugo na wafugaji ili kujua idadi yao halisi na kupanga mipango ya matumizi bora ya ardhi kulingana na mahitaji.

SEPT 21

Scanned with CamScanner

ya ujifunzaji wa ngazi ya awali ekee inaweka msisitizo katika ya kiuchumi katika jamii na ku- zo," alisema Mhagama.

NIPASHE UKIO



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega akiongea na wafugaji, wakulima wa Wilaya ya Rufiji (hawapo pichani), alipofanya ziara wilayani humo kwa lengo la kusikiliza kero na kuzitatua. Kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Meja Edward Gowelle. **PICHA: MBARAKA KAMBONA**

Scanned with CamScanner

The world seems to have forgotten impacts.

huge building complexes for health

the construction report said the

THE GUARDIAN Page 2.



Chumbi C village chairman Muhidin Mtopa (C) briefs Livestock and Fisheries deputy minister Abdallah Ulega (R, foreground) at the weekend when the latter toured an area in Rufiji District which the government has set aside as pastureland, while some portions have since been turned into residential areas and rice farms. Photo: Guardian Correspondent

Scanned with CamScanner